# Mbingu



Yerusalemu mpya , Maraika akiwa na funguo za shimo lenye kina kirefu. Picha imechorwa na , Albrecht Dürer

Je Wakristo huwa wanaenda Mbinguni wanapofariki? Mtume Paulo alisema atakapokufa ataenda kuishi na Bwana. 2(Wakorintho 5:8; Wafilipi 1:23). Kwa kuwa Bwana yuko Binguni, Paulo pia alinuia kuwa huko. Watu wengine husema anafurahia uwepo wa Mungu. Wengine wanasema amepotewa na fahamu tu. Kwa mawazo yote mawili, yeye yuko Mbinguni na Kristo.

Je, mahali hapa panapoitwa Mbinguni ni nini? Au ni mahali? Mfalme Suleimani alitambua kuwa mbingu haziwezi kumstili Mungu, na ukiangalia kimawazo tunaelezwa kuwa ndio makazi yake (1 Wafalme 8:27-30). Pamoja na kwamba Mungu hupatikana kila mahali, hayupo kila mahali katika hali moja. Kwa mfano, anaishi ndani ya wanaomwamini akiwa tofauti na anavyoishi ndani ya wasiomwamini. Tunakuja “katika uwepo wake” kwa kuutambua uwepo wake.

Maandiko yanaonyesha kuwa Mungu, pamoja na kwamba yupo kila mahali, amechagua makazi yake kuwa mbinguni – au labda tunaweza kusema wanadamu wanatumia neno mbinguni kueleza mahali pateule na patakatifu. Wanadamu walitambua kuwa Mungu haishi duniani, wala majini. Hawakuwa wanamuona angani vile vile lakini walitumia neno mbingu kueleza mahali anapotatikana Mungu.

Watu wengi walikuwa na uelewa finyu wa makazi ya Mungu na wengine walieleza makazi ya Mungu kwa upana zaidi. Pamoja na uelewa mdogo na upungufu wa maneno ya kueleza, Mungu aliwafunulia waandishi wa Biblia kutumia neno la Kiebrania na Kingiriki linalotafsiriwa kwa kiingereza kuwa mbingu ikimaanisha makazi takatifu. Wakati mwingine mbingu inatumiwa kama jina la Mungu pia, wakati mwingine likieleza utukufu wake, au nguvu zake au utakatifu wake. Kwa kweli ni mkuu kuliko mbingu lakini mbingu zinaeleza uwepo wake.

**Upungufu wa lugha.**

Hakika, kwa kuwa Mungu ni Roho, maneno yanayoonyesha umbali na vipimo yanatumika kama mfano tu. Mbingu sio juu wala chini, sio mashariki wala magharibi, haipatikani katika ramani hata ikichorwa yenye pembe zote. Kwa hivyo wakati wanadamu wanapohangaika na maelezo ya mahali, wanapojiuliza kama Wakristo huenda mbinguni wanapokufa, wanajihangaisha na swala ambalo lipo nje ya uelewa wao.

Maelezo ya kibinadamu yanayo mapungufu mengi kueleza mambo ya Kiroho. Ukichukua mfano wa upendo, raha na amani. Upendo wa Yesu unapita ufahamu (Waefeso 3:19). Mungu hutupatia raha isiyo na kifani (I Petro 1:8). Na amani yake inapita kila uelewa (Wafilipi 4:7). Maneno ya kueleza ukweli wa Kiroho huwa wanadamu hatuna. Kama kweli kueleza upendo, furaha na amani kikamilifu tunashindwa, ni kiasi gani tutapungukiwa tutakapotakiwa kueleza uwepo wa Mungu?

Mwanafilosofia mngiriki aitwaye Plato alieleza fumbo lililo onyesha dhahiri mapungufu yetu ya kueleza mambo ya Kiroho. Alieleza kuwa kulikuwa na jamii moja waliyoishi maisha yao yote ndani ya pango. Uhusiano wao na jamii zingine ulikuwa tu walipoviona vivuli chao ukutani. Wao walijua rangi nyeupe na nyeusi tu. Plato akauliza je, mmoja wao angepata ujasiri akatoka kutoka kwenye pango, akaona ulimwengu uliojaa rangi tofauti tofauti, miguso tofauti tofauti, harufu tofauti tofauti, vina na uzito, angewezaje kuwaelezea kwa lugha ya kueleweka na wenzake aliowaacha kwenye pango? Hakika ingekuwa ngumu sana kwake kueleza harufu nzuri ya kahawa, joto litokanalo na jua, jua kwao ingekuwa kama maelezo yasiyowezekana, je ziwa nalo? Lingekuwa kama tamdhilia ya abunuasi.

Vivyo hivyo, nasi tunaishi katika ulimwengu wenye mapungufu mengi ya kuelezea mambo ya Kiroho. Huwa tunaona kipengele kidogo sana cha uhalisia. Japo tunasikia kuwa ulimwengu wa Kiroho upo, hatuuoni wala kuuchunguza inakuwa ngumu. Wanaouacha ulimwengu huu na kuishi maisha baada ya kifo huwa hawarejei. Ni Yesu peke yake ambaye alivuka mpaka huu.

Ni watu wachache ambao wameona utukufu wa Mungu. “…Mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu) mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu.” (I Wakorintho 2:10) Kwa hali hiyo tunatakiwa kukiri mapungufu yetu tunapojadili maisha yetu ya milele na Mungu wetu.

**Uharisia wa Kiroho**

Mbingu ndio makao ya Roho. Paulo anaposema kuwa Mungu "ametubariki katika ulimwengu wa Kiroho" (Waefeso 1:3), haongelei kuhusu mahali, wala maisha ya usoni. Bali anaongelea uharisia wa Kiroho – Baraka za Kiroho hapa tulipo na wakati huu (Fungu hilo hilo). Anaposema tumeketi pamoja na Kristo mbinguni (Waefeso 2:6), haongelei kuhusu mahali. Bali anaongelea uharisia wa Kiroho: kwamba maisha yetu na uwepo wetu upo katika Kristo.

Katika Kristo, tunaweza kuingia mbinguni hata kabla hatujafa " Basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu." Tunaingia mbele zake sio kwa usafiri wa kimwili, bali kwa nafsi ya ndani, ndani ya roho na nafsi. Ni mwenendo wa Kiroho, sio wa kimwili, ni badiliko la fikra sio mahali.

Uraia wetu sasa uko mbinguni (Wafilipi 3:20). Hakika sisi ni wenyeji katika ulimwengu wa kiroho. Mungu anaendelea kutuvuta kuelekea mbinguni, kuelekea uharisia (Fungu 14). Kwa kuwa huku ndio kwetu, tunatakiwa kuangazia uharisia wa mbingu. Ndio maisha yetu ya usoni, na ndio wito wetu hata leo. Tunashiriki katika wito wa mbinguni; tumeonja zawadi ya mbingu (Waebrania 3:1; 6:4). Tayari tumefika Yerusalemu ya kimbingu (Waebrania 12:22) huu ndio uharisia wa Kiroho.

**Maisha ya usoni ya ajabu**

Bali bado yapo mengi yanayotusubiri. Japo tumeonja mema kutoka kwa Mungu, bado tunatamani kupata zaidi. Japo tumegusa wema wa Mungu, tunatamani kuona zaidi kidhahili na Baraka zaidi. Tunatamani kuloweshwa na upengo na mng'ao wake. Kama Ibrahimu, tunatamani mji wa mbingu (Waebrania 11:16).

Tunatamani kuwa na Mungu, ili yeye alidhishe hisia zetu za ndani. Na ndani ya miaka 10,000, tutakuwa ndio tumeanza kujifunza busara na upendo usiyo kifani. Tunayo maisha ya milele ya raha mbele yetu. "Utanijulisha njia za uzima; mbele za uso wako ziko furaha tele; na katika mkono wako wa kuume mna mema ya milele."Maneno hayatoshi kueleza wema huu. Ni furaha ya milele, amani iliyobarikiwa na utukufu wa Mungu (2 Petro 3:13).

Tumetunziwa uridhi wetu mbinguni (1 Petro 1:4). Zipo zawadi za Kiroho zinazotusubiri. "Nyumba" ya milele imetunzwa kwa ajili yetu (2 Wakorintho 5:1; Yohana 14:2-3). Haya ndio yatakayokuwa makazi yetu na ndio maana neno mbingu linatumika kama mahali tutakapofikia katika maisha ya milele kwa walio okolewa. Kuwa mbinguni ni kumbaki ndani ya Kristo ndani ya Mungu. Bila kujali ni wapi, itakuwa mbinguni na tutakuwepo.

“Maana katika nyumba hii twaugua, tukitamani sana kuvikwa kao letu litokalo mbinguni” (2Wakorintho 5:2). Tumechoshwa na maumivu na dhiki na mateso ya ulimwengu huu. Tuna “ugua” kindani ndani tunapongojea kunyakuliwa na kufanywa wana, kuokolewa kwa miili yetu (warumi 8:23). Hata hivyo, tunasubiri kwa uvumilifu, (fungu 25), tukijua hivi karibuni hakutakuwepo kifo, dhiki, kilio na maumivu (Ufunuo 21:3-4; 22:1-5).

Tutakapo fufuliwa, tutakuwa na miili ya Kiroho, (1Wakorintho 15:44) kwa njia moja au nyingine tutakuwa kama Kristo wakati wa ufufuo wake (1Yohana 3:2). Itakuwa maisha ya mbingu katika uharisia wote. “ na kama tulivyoichukua sura yake yule wa udongo, kadhalika tutaichukua sura yake yeye aliye wa mbinguni.” (1 Wakorintho 15:49). Tutakuwa wana wa “mbingu” (Fungu 48).

Zawadi za mbingu zitakuwa zetu kufurahia milele. Haijalishi tunaanza kuhisi utukufu huo lini. Mahali itakapokuwa pia sio muhimu. Jambo la muhimu ni kuwa na Bwana milele (1 Wathesalonike 4:17). Na la muhimu zaidi ni kupitia kwa Bwana wetu, na kupitia kwake tu ndio tunaweza tu kuwepo. Ni kwa neema ndio tunaweza kuingia ufalme wa mbinguni.

Lakini shukrani kwa Mungu, kwa kuwa ametupatia ushindi. Katika Kristo, maisha yetu ya baadaye yamehakikiwa. “Bwana ataniokoa na kila neno baya, na kunihifadhi hata nifike ufalme wake wa mbinguni. Utukufu una Yeye milele na milele. Amina” (2 Timotheo 4:18).